




Zama ni mkubwai!



Michael Oguttu ✎
Vusi Malindi 🗣️
Matteo E. Mwita 📖
Kiswahili 😊
Level 2 📖

(imageless edition)



Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Zama ni mkubwai!

Written by: Michael Oguttu


Illustrated by: Vusi Malindi

Translated by: Matteo E. Mwita

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.




This work is licensed under a Creative Commons Attribution 3.0 International License.
<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>



Mdogo wangu anachelewa kuamka.
Mimi naamka mapema kwa sababu
mimi ni mkubwa!

Mimi ndiye ninayeruhusu jua kuingia ndani.






“Wewe ni nyota wangu wa asubuhi,”
anasema mama.




Ninafanya hivi vitu vyote vizuri kila
siku. Ila kitu ninachokipenda sana ni
kucheza na kucheza.

Darasani najitahidi sana katika kila kitu.




Naoga mwenyewe, sihitaji msada.







Naweza kustahimili maji ya baridi na sabuni ya bluu inayonuka.



Na ninahakikisha mdogo wangu anapata taarifa zote za shule.




Mama ananikumbusha, "Usisahau kupiga mswaki." Namjibu, "Kamwe, sio mimi!"



Ninaweza kufunga vishikizo na kurekebisha viatu vyangu.



Baada ya kuoga, nawasalimu babu na shangazi, na kuwatakia siku njema.



Najivisha nguo mwenyewe. "Mimi ni mkubwa sasa mama," ninamwambia.